East African Journal of Swahili Studies, Volume 7, Issue 1, 2024
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2066

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 7, Issue 1, 2024
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Upya wa Utenzi wa Mwana Kupona katika utenzi wa Howani Mwana Howani na Jawabu la Mwana Kupona

*Gladys Kinara[1*] Dkt. Richard Makhanu Wafula, PhD[1] na Dkt. Pamela Muhadia Y. Ngugi, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kenyatta, S. L. P. 43844-00100, Nairobi, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: glamoke@yahoo.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2066**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*29 Julai 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Ufeministi wa Kiafrika, Haki za Wanawake.*

**IKISIRI**

Makala hii ililenga kuchunguza upya wa *Utenzi wa Mwana Kupona* katika utenzi wa *Howani Mwana Howani* na *Jawabu la Mwana Kupona*. Makala hii iliongozwa na nadharia ya Bakhtin kuhusu lugha (1981) na Ufeministi wa Kiafrika iliyoasisiwa na Chioma (1980). Nadharia ya Bakhtin kuhusu lugha inashikilia kuwa lugha huwa na kani za aina mbili: nguvu za Kani Kitovu na Kani Pewa. Nguvu za Kani Kitovu zinafanya kazi kwa kuvuta vipengele vyote vya lugha na mbinu zake za ufasaha kuelekea katikati ili kutoa lugha moja iliyo sanifu au rasmi ambayo kila mmoja anaitumia. Nguvu hizo za Kani Kitovu zilikuwa kanuni zilozounganisha na kuleta kitu katikati. Nguvu za Kani Pewa zilijaribu kusukuma vipengele vya lugha kutoka katikati na kupelekea kuwa na wingi wa lugha au vijilugha. Kwa upande mwingine, Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika iliasisiwa katika miaka ya 1980 na Chioma na Kuendelezwa na Ogundipe (1994), Nnaemeka (2003) miongoni mwa wengine. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inafafanuliwa kama mapambano dhidi ya aina zote za dhuluma ili kupiga hatua katika kupata haki za wanawake. Jitihada hizi zinaweza kuwa za kijinsia, ubaguzi wa rangi, unyanyasaji wa kiuchumi kati ya dhuluma nyinginezo zinazolenga kumdhalilisha mwanamke (Bayu, 2019). Utafiti ulikuwa wa kimaelezo. Utafiti ulifanywa maktabani na nyanjani. Sampuli maktabani na nyajani iliteuliwa kimaksudi. Maktabani, mtafiti alisoma kwa kina matini iliyochapishwa kwa lengo la kupata data ya msingi. Nyanjani, mtafiti alifanya mahojiano na majadiliano na wanajamii walioteuliwa katika kukusanya data. Data kutoka katika tenzi zilizoteuliwa, maandishi yaliyohusu utafiti huu, data ya nyanjani zilichambuliwa kulingana na lengo la makala haya na mihimili ya nadharia kwa lengo la kuonyesha namna upya wa Mwana Kupona ulivyobainika katika utenzi wa *Howani Mwana Howani* na *Jawabu la Mwana Kupona*. Makala haya yalibainisha kuwa utenzi wa *Howani Mwana Howani* na *Jawabu la Mwana Kupona* zilisheheni upya kifani na kimaudhui katika mpito wa wakati.

**APA CITATION**

Kinara, G., Wafula, R. M. & Ngugi, P. M. Y. (2024). Upya wa Utenzi wa Mwana Kupona katika utenzi wa Howani Mwana Howani na Jawabu la Mwana Kupona. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 343-358. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2066.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**CHICAGO CITATION**

Kinara, Gladys, Richard Makhanu Wafula and Pamela Muhadia Y. Ngugi. 2024. "Upya wa Utenzi wa Mwana Kupona katika utenzi wa Howani Mwana Howani na Jawabu la Mwana Kupona". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 343-358. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2066

**HARVARD CITATION**

Kinara, G., Wafula, R. M. & Ngugi, P. M. Y. (2024) "Upya wa Utenzi wa Mwana Kupona katika utenzi wa Howani Mwana Howani na Jawabu la Mwana Kupona", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 343-358. doi: 10.37284/jammk.7.1.2066

**IEEE CITATION**

G. Kinara, R. M. Wafula & P. M. Y. Ngugi "Upya wa Utenzi wa Mwana Kupona katika utenzi wa Howani Mwana Howani na Jawabu la Mwana Kupona", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 343-358, Jul. 2024.

**MLA CITATION**

Kinara, Gladys, Richard Makhanu Wafula & Pamela Muhadia Y. Ngugi. "Upya wa Utenzi wa Mwana Kupona katika utenzi wa Howani Mwana Howani na Jawabu la Mwana Kupona". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, Jul. 2024, pp. 343-358, doi:10.37284/jammk.7.1.2066.

## UTANGULIZI

Makala hii yanalenga kuchunguza upya wa *Utenzi wa Mwana Kupona* (Allen, 1971) katika utenzi wa *Howani Mwana Howani* (Mohammed, 1983) na *Jawabu la Mwana Kupona* (El-Maawy, 2011). Mdee, Njogu na Shafi (2011) wanaeleza upya kama mabadiliko yanayotokea katika kazi ya fasihi kando na yale asilia katika mpwito wa wakati. Upya huu unaweza kutokea kwa njia na viwango anuwai. Unaweza kutokana na mwingiliano matini unaoleta mwangwi, mahusiano ya matini, wizi wa maandishi, mwangwi wa kifasihi, utohozi wa kifasihi, uhamishaji wa fasihi au marekebisho ya kifasihi.

Katika fasihi ya Kiswahili, mapokeo na upya yameonyeshwa katika uhusiano kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. Fasihi Andishi kwa kiasi kikubwa iliazima kutoka katika kazi za fasihi simulizi (Wamitila, 2003). Kwa hivyo, mapokeo yanakuwa kazi ya fasihi simulizi nayo fasihi andishi inakuwa upya. Katika muktadha wa utafiti huu, mapokeo ni utamaduni wa Waswahili kama unavyoonyeshwa na *Utenzi wa Mwana Kupona* wa karne ya 18 na 19 nao upya ni mabadiliko yanayotokea katika kazi za sanaa zilizosimilishwa au zinazofanana kidogo na zilizochapishwa baada ya *Utenzi wa Mwana Kupona*. Ni nadra kupata kazi zilizotafitiwa kuthibitisha mapokeo haya katika kazi za fasihi andishi ya Kiswahili. Ni katika muktadha huu ambapo makala haya yalilenga kuchunguza namna *Utenzi wa Mwana Kupona* ulivyoendelea kunyumbuliwa na waandishi wa baadaye. Mabadiliko waliyoleta katika tenzi za *Howani Mwana Howani uliotungwa* na Zainab Himid Mohamed mwaka wa 1983 na utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona* uliotungwa na Ali Abdalla Ali El-Maawy mwaka wa 2011 yakakuwa upya na yale waliyoazima kutoka katika *Utenzi wa Mwana Kupona* yakakuwa mapokeo.

### Suala la Utafiti

*Utenzi wa Mwana Kupona* ni utenzi maarufu na mkongwe na umeshughulikiwa na wataalam mbalimbali. Utenzi huu ulitungwa mwaka wa 1858. Tangu wakati huo, tenzi nyingine zimetungwa ambazo kwa njia moja au nyingine zinarindima mwangwi wa *Utenzi wa Mwana Kupona*. Hizi ni pamoja na utenzi wa *Howani Mwana Howani* Mohammed (1983) na *Jawabu la Mwana Kupona* El- Maawy (2011). Ni katika muktadha huu ambapo makala hii ililenga kuchunguza namna *Utenzi wa Mwana Kupona* unavyobainika katika upya wa *Howani Mwana Howani* na *Jawabu la Mwana Kupona*.

## YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Sehemu hii imeshughulikia uhakiki wa yaliyoandikwa kuhusu mada. Sehemu ya kwanza imeshughulikia tahakiki za *Utenzi wa Mwana Kupona* (Allen, 1971) kwa lengo la kubaini pengo la makala husika. Sehemu ya pili ilichunguza upya unaobainika katika tahakiki za warithi wa *Utenzi wa Mwana Kupona* zikiwemo kazi za Zaynab Himid Mohammed (1983) na El-Maawy, A. (2011).

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2066

### Tafiti kuhusu Utenzi wa Mwana Kupona

Kuna tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu *Utenzi wa Mwana Kupona*. Taz: Strobel, (1979) Njozi (1990), Khatib (1985) Biersteker, (1991) Swaleh, (1992) Gibbe, (1995), Wandera (1996), Mulokozi (1999), Momanyi (2007), Beja na Mwinyifaki (2013) Timammy na Swaleh (2013) na Munyole (2017). Tafiti hizi zilitumia nadharia tofauti zilizoafikiana na malengo ya kila mtafiti. Hata hivyo kazi hizo za awali kuhusu *Utenzi wa Mwana Kupona* zilikuwa muhimu katika kubainisha pengo la makala haya ambayo yalilenga kuchunguza upya wa *Utenzi wa Mwana Kupona* katika upya wa *Howani Mwana Howani* na *Jawabu la Mwana Kupona*.

### Tafiti kuhusu utenzi wa Howani Mwana Howani (1983) na *Jawabu la Mwana Kupona* (2011).

Kuna tafiti zilizofanywa kuhusu *utenzi wa Howani Mwana Howani* uliotungwa na Zaynab Himid Mohammed (1983). Mbayi (2009) alichunguza fani katika utenzi wa *Howani Mwana Howani* na *Mwanakukuwa* zilizotungwa na Zaynab Himid Mohammed mwaka wa 1983. Aliongozwa na nadharia ya umuundo ambayo ilimsaidia kuhakiki vipengele vya fani kimatini bila kulazimika kuwa na urejelezi wowote wa nje. Utafiti huo ulibaini namna msanii alivyotumia vipengele vya fani kujenga kazi zake mbali na kutoa mifano ya kila kipengele katika muktadha wa utenzi wa *Howani Mwana Howani* na *Mwanakukuwa*. Naye Mohamed (2016) alifanya utafiti kuhusu mila na desturi za mwanamke wa visiwani katika diwani ya *Howani Mwana Howani* ambayo ina utenzi wa *Howani Mwana Howani* na *Mwanakukuwa.* Aidha, alichunguza vipengele vya fani vikiwemo matumizi ya lugha, mandhari na wahusika. Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya sosholojia na semiotiki. Tofauti na utafiti wa Mbayi na Mohammed, makala haya yalitumia nadharia ya Bakhtin kuhusu lugha na Ufeministi wa Kiafrika. Aidha, yalichunguza upya wa *Utenzi wa Mwana Kupona* katika upya wa utenzi wa *Howani Mwana Howani* na utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona.*

### Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Ki-Bakhtin kuhusu lugha na nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Nadharia hizi zilisaidia katika kutekeleza malengo ya makala haya ambayo yalikuwa kujadili upya wa *Utenzi wa Mwana Kupona* katika utenzi wa *Howani Mwana Howani* (1983) na *Jawabu la Mwana Kupona* (2011).

### Nadharia ya Bakhtin kuhusu Lugha

Nadharia hii iliasisiwa na Mikhail Bakhtin (1981) ambaye alikuwa Mwanafalsafa wa Kirusi. Aliandika kazi zake katika miaka baada ya mapinduzi ya Urusi ya 1917. Kazi za Bakhtin ziliendelezwa na kusambazwa na baadhi ya wahakiki wakiwemo: Hirschkop (2001), Holquist (2002) na Brandist (2002) kati ya wengine. Bakhtin aliazima maneno haya kutoka katika somo la Fizikia. Katika somo hilo la Fizikia, Kani Kitovu ni sehemu ya nguvu inayoelekezwa kwenye kitovu au katika mhimili mkuu wa mzunguko. Nguvu za Kani Pewa nazo ni kinyume cha nguvu za Kani Kitovu zinazovuta kwenda nje ya kitovu. Nguvu za Kani Kitovu na nguvu za Kani Pewa ni maneno ya Kirusi yaliyotafsiriwa katika lugha ya Kiingereza na kisha baadaye katika Kiswahili katika kamusi ya Bayoloji, Fizikia na Kemia (Wamitila, 2002).

Bakhtin (1981) anasema, nguvu za Kani Kitovu zilifanya kazi kwa kuvuta vipengele vyote vya lugha na mbinu zake za ufasaha kuelekea katikati ili kutoa lugha moja iliyo sanifu au rasmi ambayo kila mmoja alizungumza na kuitumia. Nguvu hizo za Kani Kitovu zilikuwa kanuni zilizounganisha na kuleta kitu katikati. Katika muktadha wa kazi hii, nguvu za Kani Kitovu ziliwakilisha utamaduni wa Waswahili kama unavyoonyeshwa na *Utenzi wa Mwana Kupona* wa wakati wa karne ya 18 na 19.

Kwa upande mwingine, nguvu za Kani Pewa zilijaribu kusukuma vipengele vya lugha kutoka katikati na kupelekea kuwa na wingi wa lugha au vijilugha. Kwa kuwa nguvu hizi zilivuta kwenda nje zilidengua, ziliweka katika tabaka na zilienda kinyume na kanuni za Kani Kitovu. Katika

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2066

muktadha wa fasihi, matini ambayo iliathiriwa na nguvu za Kani Pewa iliendelea kubadilika kila wakati. Mabadiliko haya yaliwakilisha upya ambao ulitokea katika kazi za sanaa zilizosimilishwa au zinazofanana kidogo na zile ilizochapishwa baada ya *Utenzi wa Mwana Kupona*. Katika Muktadha huu utenzi wa *Howani Mwana Howani* (1983) na *Jawabu la Mwana Kupona* (2011).

Asemavyo Wamitila (2002), Kani Kitovu na Kani Pewa ni dhana zinazohusishwa na Mikhail Bakhtin aliyezitumia kuelezea mvuto wa kutoka nje ya kitovu fulani. Kani hizi kwa mujibu wa Bakhtin (1981), zinapatikana katika lugha. Kwa mfano, kuna mvuto kuelekea kwenye usawawishaji wa lugha unaoshikiliwa na kundi fulani na wakati uo huo mvuto wa kiusambazaji ili kuonyesha sauti mbalimbali. Bakhtin anaamini kuwa, kuna tanzu fulani ambazo zina mwelekeo wa Kani Kitovu yaani kumvuta msomaji kwenye ukubalifu fulani na nyingine ambazo zina Kani Pewa au zinazohimiza tofauti na wingi sauti.

Nadharia hii itachunguza upya unaobainika katika tenzi za za *Howani Mwana Howani* (1983) na utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona* (2011). Hata hivyo, ijapokuwa tenzi hizi zimebainisha upya, kuna baadhi ya maudhui ambayo yanaonekana kuwa yana mwangwi wa *Utenzi wa Mwana Kupona* (Allen, 1971). Sehemu itakayofuata itashughulikia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Nadharia hii itasaidia katika kuhakiki maudhui ambayo ijapokuwa yameshughulikiwa katika upya wa tenzi za *Howani Mwana Howani* (1983) na utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona* (2011) yana mwangwi wa *Utenzi wa Mwana Kupona*.

**Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika**

Tong (2009), anafafanua ufeministi kama harakati ya ulimwengu mzima inayolenga kuinua hali ya wanawake kisiasa, kiuchumi na kijamii na kupigania usawa wa kijinsia katika nyanja zote za maisha katika jamii zote. Vivyo hivyo, ufeministi unalenga kuwakomboa wanawake kutokana na dhuluma za aina yote na kuleta mshikamano wa wanawake wa mataifa yote (Beasley, 1999).

Ufeministi wa Kiafrika ni nadharia iliyoasisiwa katika miaka ya 1980 na Chioma na Kuendelezwa na Ogundipe (1994), Nnaemeka (2003 na 2013) miongoni mwa wengine. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inafafanuliwa kama mapambano dhidi ya aina zote za dhuluma ili kupiga hatua katika kupata haki za wanawake. Jitihada hizi zinaweza kuwa za kijinsia, ubaguzi wa rangi, unyanyasaji wa kiuchumi kati ya dhuluma nyinginezo zinazolenga kumdhalilisha mwanamke (Bayu, 2019). Nadharia hii itachangia katika kuchunguza baadhi ya maudhui ambayo japo yanadhihirisha mapokeo ya *Utenzi wa Mwana Kupona*, yana upya wake katika upya wa tenzi za *Howani Mwana Howani* (1983) na utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona* (2011).

Baadhi ya mihimili ya nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ni kama vile dhana ya uanawake (womanism) kama inavyofafanuliwa na Ogunyemu (1985) na Kolawale (1997). Neno hili limetumiwa na Wafeministi katika kushughulikia wanawake Waafrika ili kukabiliana na utamaduni, ukoloni na mambo mengine mengi yanayotawala maisha ya wanawake wa Kiafrika. Pia, kuna mabadiliko ya kijamii yanayowahusisha wanawake wa Kiafrika. Dhana hii ilibuniwa na Ongudipe (1994) kutokana na maneno ya Kiingereza STWA (Social Transformation Including Women in Africa). Mhimili mwingine ni 'ukinamama' (Motherism) (tafsiri yetu) kama lilivyofafanuliwa na Acholonu (1995), neno hili 'ukinamama' lilipanua mtazamo wake kwa wanawake wa Kiafrika kwa kuwapa wanawake wa vijijini au mashambani jukumu la kuikimu jamii. 'Ufeministi wa hisia ya konokono' (snail sense feminism) kama ilivyofafanuliwa na Ezeigbo (2012) anasema ni kutumia mwendo wa konokono ili kujadiliana na mume kwa lengo la kutatua matatizo ya kinyumbani kwa kutumia ulimi mtamu, ili kukabiliana na changamoto za nyumbani hata ziwe ni za kiwango kipi na 'Ufemali' (Femalism) kama anavyofafanua Opara (2005) anatazama dhana hii kwa kuilinganisha na mwili wa mwanamke unavyodhulumiwa. Maumbile ya mwanamke yanakuwa ndio chanzo cha udhalimu. Hata hivyo, nadharia hii inajaribu kukiuka mielekeo hiyo hasi inayotazama mwili

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2066

wa mwanamke kama usiokuwa na thamani na badala yake kutoa njia chanya ambazo zinaweza kutumiwa kuusawiri mwili wa mwanamke. Mihimili hii ilituwezesha kuhakiki tenzi husika kwa lengo la kuchunguza tamaduni zilizokuwa muhimu kuhifadhiwa katika jamii katika muktadha wa Kiafrika mbali na kukumbatia upya uliotokea katika jamii.

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo. Utafiti ulifanywa maktabani na nyanjani. Maktabani, mtafiti alisoma kwa kina matini iliyochapishwa kwa lengo la kupata data ya msingi. Nyanjani, mtafiti alifanya mahojiano na majadiliano na wanajamii. Sampuli ya maktabani na nyanjani iliteuliwa kimaksudi. Maktabani, mtafiti alisoma vitabu, tahakiki, tasnifu kwa lengo la kupata pengo la makala haya na data ya msingi. Nyanjani, mtafiti aliteua wasailiwa watano ambao walikuwa na umri tofauti, elimu na jinsia tofauti kutoka katika jamii ya Lamu. Mtafiti alitumia mwongozo wa maswali na mijadala kama nyenzo kuu katika ukusanyaji wa data ya upili. Data ya nyanjani na maktabani iliainishwa kulingana na namna upya wa Mwana Kupona ulivyobainika katika upya wa utenzi wa *Howani Mwana Howani* na *Jawabu la Mwana Kupona*.

## UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA MATOKEO.

Sehemu hii itashughulikia uchanganuzi wa matokeo katika utenzi wa *Howani Mwana Howani* na *Jawabu la Mwana Kupona k*wa kuchunguza upya wa tenzi husika katika muktadha wa *Utenzi wa Mwana Kupona*. Sehemu ya kwanza itashughulikia *Utenzi wa Howani Mwana Howani* Mohammed (1983) nayo sehemu ya pili itashughulikia utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona* El-Maawy (2011).

### Wasifu wa Zaynab Himid Mohammed

Utenzi wa *Howani Mwana Howani* ulitungwa na Zaynab Himid Mohammed mwaka wa 1983. Bi. Zaynab Himid Mohammed alizaliwa tarehe 12 Februari, mwaka wa 1918 katika mtaa wa Mkocheni huko Malindi nchini Kenya. Baadaye babake alihamia Zanzibar kwa ajili ya kazi. Alianza shule tarehe 1 Juni, 1927 huko Forodhani-Zanzibar. Alikuwa miongoni mwa wasichana wachache wa Kiafrika walioanza kusoma shule huko Zanzibar. Mwaka wa 1934, Bi Zaynab alikuwa miongoni mwa wanafunzi wa mwanzo kufaulu kupata nafasi ya mpango wa “pupil teacher” yaani “mwalimu mwanafunzi” ambapo alisoma masoma ya darasa la saba na nane kwa baadhi ya masaa, huku akisoma mafunzo ya ualimu muda uliosalia.

Mwaka wa 1936 Januari, alianza kazi ya ualimu katika shule maarufu ya Town Primary mjini Unguja, akiwa na wanafunzi 16. Alianza kwa kutunga utenzi wa *Howani Mwana Howani* kisha baadaye akatunga *Utenzi wa Mwana Kukuwa* kwa ajili ya kumbukumbu ya mama yake Mwana Kukuwa ambao kwa pamoja ulichapishwa mwaka 2004 katika diwani yake ya *Howani Mwana Howani*. Mwaka uo huo wa 1936, aliolewa na mtoto wa shangazi yake akiwa na miaka 18. Baadaye ndoa hiyo haikufaulu. Kulingana na Othman na Yaya katika dibaji ya diwani ya *Howani mwana Howani*, Zaynab Himid aliwahi kuolewa mara tatu, lakini hakubahatika kupata watoto. Aliwachukua watoto wa ndugu yake akawalea kama wake. Japo Zaynab hakubahatika kupata watoto, kama mwalimu, aliwapenda watoto. Kule nyumbani kulikuwa kumejaa watoto kutoka mashambani (mikoani kwa lugha ya Tanzania bara) na Pemba ambao wazee walimkabidhi ‘Bi Mwalimu’ awafundishe.

Tajriba ya mwandishi ndiyo iliathiri utunzi wake hasa kutokana na sababu kuwa alikuwa amepata elimu ya Magharibi na mwalimu mwenye tajriba katika masuala ya elimu ya Kimagharibi ya wakati wake. Aliona athari ya elimu ya Kimagharibi na hivyo akaona haja ya kuhifadhi utamaduni wa Waswahili ili usije ukasahaulika kutokana na ujio wa elimu ya Kimagharibi.

Sehemu inayofuata itachunguza upya wa utenzi wa *Howani Mwana Howani* Mohammed (1983) ukiwemo dhamira ya mtunzi, maudhui mapya katika uenzi huo kama vile malezi ya mimba na kujifungua, malezi ya mtoto mchanga, tiba za

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2066

kienyeji, sherehe za Waswahili na vipengele vya fani vikiwemo muundo mazingira na wahusika.

**Dhamira ya Mtunzi**

Utenzi wa *Howani Mwana Howani* ulitungwa na Bi. Zaynab Himid Mohammed mwaka wa 1983. Utenzi huu ulitungiwa bintiye mlezi Sihadaike kwa lengo la kuhifadhi utamaduni wa Mswahili hasa baada ya ujio wa elimu ya Kimagharibi. Kulingana na Mohammed (1983), Mtunzi anasema alihadithiwa mambo mengi aliyoandika katika tenzi zake na mama yake alipokuwa mchanga na mengine alimfundisha alipokuwa kigori hadi alipoolewa. Kwa hivyo, yeye alichota maudhui yake kutokana na yale aliyohadithiwa na kufundishwa na mama yake. Dhamira yake ilikuwa kuhakikisha kuwa aliyohadithiwa na aliyofundishwa hayakusahaulika. Pia, alipotoa shukrani kwa nduguye Salim Himid Mohammed, alisema kuwa, yeye alimpa moyo kutunga tenzi hizo zilizomkumbusha mambo yaliyokuwa hapo kale.

Mohammed (1983) katika utenzi wa *Howani Mwana Howani* na Mwana Kupona katika *Utenzi wa Mwana Kupona* Allen (1971) walikuwa wa jinsia moja na walilenga kuwaasa watoto wa kike katika utunzi wao. Aidha, utamaduni uliokusudiwa kuhifadhiwa ulikuwa mapokeo ya wanajamii kwa kuwa Mwana Kupona na Bi. Zaynab walilenga kuhifadhi mafundisho ya kijamii yaliyowahusu mabinti. Vilevile, Zaynab na Mwana Kupona waliwatakia watoto wao makuzi mema. Hii inaonyesha kwamba nguvu za Kani Kitovu zilifanya kazi kwa kuwaleta pamoja hasa kuhusu mafundisho ya watoto wa kike ijapokuwa watunzi hawa waliishi katika karne tofauti kiwakati mbali na kuwa walikuwa na tajriba tofauti kuhusu masuala ya elimu ya wakati wao kama toleo la nguvu za Kani Pewa (Bakhtin, 1981)

**Malezi ya Mimba na Kujifungua**

Kulingana na Mohamed (1983), malezi ya uja uzito yalikuwa sehemu muhimu ya utamaduni wa Mswahili. Malezi haya yalianza pindi mke alipopata mimba. Ikumbukwe kuwa, katika kipindi cha utenzi, hapakuwa na daktari wa kubaini ni kitu kipi kilichomsumbua mama (Mohammed, 1983:- ubeti, 14). Kulingana na mila na desturi za Waswahili, mama alitunza mimba hiyo hadi miezi mitatu kwa sababu katika kipindi hicho, mimba ilihitaji makini katika kuitunza. Mama alikatazwa kufanya kazi nyingi ili mimba isiharibike ikizingatiwa kuwa hapakuwa na daktari wa kumtahadharisha kuhusu kazi nyingi. Kwa hivyo wanajamii waliwajibika kwa kutompa mama kazi nyingi (Mohammed, 1983).

Utamaduni huu wa Mswahili unashadidiwa na mawazo ya Mbaabu (1985) ambaye anasema kuwa, mwanamke apatapo mimba gharama kubwa humfikia Mswahili katika kulea ile mimba. Wakati mke ana mimba ya miezi mitano hivi, bwana huwa hapendi mke wake afanye kazi yoyote ile. Utamaduni huu wa Mswahili wa kulea mimba unabainisha upya wa kimaudhui tofauti na yale aliyoangazia Mwana Kupona. Aidha, unaonyesha nafasi ya pekee anayopewa mwanamke katika jitihada zake za kuleta uhai katika jamii. Opara (2005) akifafanua katika nadharia yake ya 'Ufemali', anabainisha namna mwili wa mwanamke unavyodhulumiwa. Maumbile ya mwanamke yanakuwa ndio chanzo cha udhalimu. Hata hivyo nadharia hii inajaribu kukiuka mielekeo hiyo hasi inayotazama mwili wa mwanamke kama usiokuwa na thamani na badala yake kutupa njia Mohammed (1983) anatazama jukumu la malezi ya mimba kama sehemu muhimu ya mwanamke kwa kuleta kiumbe ulimwenguni kwa hivyo ni suala ambalo linastahili kupewa heshima.

**Malezi ya Mtoto Mchanga**

Katika utamaduni wa Waswahili, baada ya mtoto kuzaliwa alisafishwa vizuri na kuvalishwa nguo, baadaye alilazwa kwenye ungo uliotandikwa kanga kama kigodoro cha kulalia na mto wake ulikuwa ni mchanga. Mto huu ulikuwa katika utamaduni wa Waswahili tangu jadi na lengo lake lilikuwa kutengeneza kisogo cha mtoto (Mohammed, 1983:- ubeti, 60 na 61). Siku ya arobaini wazazi wa kuumeni na kuukeni huwa na sherehe ya kumtoa nje mzazi na mjukuu wao.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2066

Baada ya kutolewa nje, hupewa jina. Baada ya hapo, mzazi na mtoto wake huwekwa huru kutoka nje. Mtoto wa kike wa visiwani pia alipakwa wanja machoni ili atakapokuwa mkubwa awe na haya usoni. Lengo lingine la kumpaka wanja lilikuwa ni kuficha sura yake halisi ili aepukane na mahasidi wa mdomo na kijicho (Mohammed, 1983:- ubeti, 130 na 131).

Kulingana na nadharia ya Bakhtin (1981), nguvu za Kani Pewa za lugha ziliathiri msamiati. Katika muktadha wa fasihi, nguvu hizi zilionekama kuathiri matini kwa kuifanya kubadilikabadilika. Katika muktadha huu, nguvu za Kani Pewa zilituwezesha kuchunguza mabadiliko yaliyotokea katika utenzi wa *Howani Mwana Howani* (1983). Utenzi huu ulionekana kuwa na upya kutokana na yale aliyoangazia mtunzi. Mohammed (1983) aliangazia suala la malezi ya mtoto mchanga katika muktadha wa jamii ya Waswahili kwa kuangazia mila na desturi walizofanya Waswahili mtoto alipozaliwa. Kwa mfano, katika muktadha huu wanja ilipakwa machoni kwa lengo la kumkinga mtoto dhidi ya husuda. Mawazo haya yanabainisha upya kutokana na yale aliyoangazia Mwana Kupona kwa kuwa Mwana Kupona alimwomba bintiye kutia wanja machoni kama sehemu ya urembo. Miktadha hii tofauti ya watunzi inabainisha namna nguvu za Kani Pewa za lugha zilivyofanya kazi na kuleta tofauti katika utenzi wa *Howani Mwana Howani* na *Utenzi wa Mwana Kupona.*

**Tiba za Kienyeji**

Jamii ya Waswahili ilitumia tiba za kienyeji na ingali inatumia tiba hizi hadi sasa. Waswahili walitumia tiba hizi katika shughuli mbalimbali za maisha. Kwa mfano, mama alipokuwa mja mzito alipewa dawa za kienyeji. Aidha, walitumia mafuta ya ufuta kupaka tumboni mwa mama mja mzito (Mohammed, 1983:- 28 na 29). Ilipofika wakati wa kujifungua, mivuje ilichemshwa na kuchanganya na dawa iliyoitwa habasodi. Aidha, habasodi nyingine ilitiwa kwenye kikombe na kupewa mama mjamzito anywe (Mohammed, 1983:-ubeti, 45).

Akishadidia haya, Mohammed (2016) anasema kuwa, dawa nyingine walizotumia Waswahili ni kama mizizi, majani, matunda ya mimea, mafuta ya nazi au ya alizeti ambayo ilichanganywa na dawa nyingine kama tiba ya magonjwa mbalimbali. Vilevile, dawa za kunywa zilimsaidia mgonjwa kuondoa maradhi yaliyo mwilini mwake na dawa za kufukiza zilitumika kwa lengo la kufukiza mashetani.

Ijapokuwa maudhui haya ya tiba za kienyeji ni ya kimapokeo, Mwana Kupona hakushughulikia utamaduni huu wa Mswahili; badala yake aliangazia masuala ya unyumba. Mohamed (1983), anasema, ulimwengu tunamoishi sasa umegubikwa na wingu la mabadiliko ambayo mengine ni ya ghafla na yenye sura ya mapinduzi. Kulingana naye, kuna mapinduzi ya fikra na yale ya mila nyingi za kale. Mengi ya yale waliyokuwa wakiyathamini, sasa yalionekana kama upuuzi na upotevu. Baadhi ya mambo waliyoyathamini yalififia na hata kusahaulika kutokana na majilio ya teknolojia na mabadiliko ya wakati. Kwa hivyo, Mohamed (keshatajwa) aliona haja ya kuuhifadhi kwa njia ya maandishi utamaduni wa Wazanzibari ili usizame na kupotea kabisa kwa vizazi vijavyo. Kwa hivyo, hadhira yake ilikuwa pana kuliko ya Mwana Kupona.

Ijapokuwa Mohamed (1983) aliangazia tiba za kienyeji kama sehemu ya mapokeo ya Mswahili kama toleo la nguvu za Kani Kitovu za lugha, maudhui yake yalielekea kuwa mapya tofauti na yale aliyoangazia Mwana Kupona kama toleo la nguvu za Kani Pewa za lugha kwa kuwa utamaduni huu wa tiba za kienyeji haukuangaziwa na Mwana Kupona. Aidha, kulingana na Mohamed (1983), alilenga kuhifadhi utamaduni wa Mswahili ambao ulionekana kutishiwa na maendeleo ya jamii kutokana na majilio ya teknolojia. Akishadidia haya Acholonu (1995) anatumia dhana ya Ukina mama (Motherism) (tafsiri yetu) kupanua mtazamo wake kwa wanawake wa Kiafrika kwa kuwapa wanawake wa vijijini au mashambani jukumu la kuikimu jamii. Mohammed anachukua nafasi kuhifadhi utamaduni wa Waswahili wa matumizi ya miti shamba ili kuufanya usife. Matumizi ya dawa hizi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2066

yanaonyesha nafasi muhimu waliyonayo wanawake katika kuhifadhi utamaduni huu.

**Sherehe za Waswahili**

Jamii ya Waswahili pia ilikuwa na sherehe mbalimbali. Kwa mfano, kulikuwa na sherehe za kumpa mtoto jina. Kulingana na Mohamed (1983) katika utenzi wa *Howani Mwana Howani*, mama akishajifungua, baada ya siku arobaini sherehe huandaliwa ili kumpa mtoto jina. Wazee hualikwa katika sherehe hiyo. Aidha, siku ya kwanza kumpeleka mtoto shuleni sherehe hufanywa. Baada ya mtoto kumaliza masomo ya unyago au tohara, sherehe huandaliwa. Binti anapoolewa au mwana anopooa sherehe huandaliwa. Shughuli nyingi katika jamii hii huwa na sherehe ila tu suala la kiuchumi liwazuie kuandaa sherehe hizo. Vilevile, kulikuwa na sherehe za jando na unyago. Mtoto wa kiume alipofanyiwa tohara alipotimia umri wa kuelewa na kupambanua mambo vizuri. Waaidha, baada ya mtoto wa kike kupelekwa unyagoni, sherehe iliandaliwa.

Ijapokuwa sherehe hizi za Waswahili ni suala la kimapokeo ambalo linatokana na nguvu za Kani Kitovu, Mwana kupona hakulishughulikia. Kwa hivyo, maudhui haya ya sherehe za Waswahili yanabainisha upya kama toleo la nguvu za Kani Pewa kwa kuwa ni tofauti na maudhui aliyoshughulikia Mwana Kupona. Mwandishi alichukua jukumu la kuhifadhi utamaduni wa Waswahili kwa kina.

**Vipengele vya Muundo katika Utenzi wa *Howani Mwana Howani***

Baadhi ya vipengele vya fani kati utenzi wa *Howani Mwana Howani* (1983) ni kama vile muundo, mazingira na wahusika. Mtunzi ameuanza utenzi wa *Howani Mwana Howani* kwa kumhutubia mwanawe moja kwa moja bila kutumia fomula ya kawaida ya utangulizi wa tenzi. Watunzi huanza kwa shukrani za Maulana na kisha kuomba wino, kalamu na karatasi ya kuandika. Baadaye, huwa wanasifia Mwenyezi Mungu kwa maajabu ya viumbe vyake, kutoa dua na heshima zao kwa Mtume Mohammed na jamii yake. Mtunzi alikiuka mazoea hayo (Mohammed, 1983:- ubeti, 2 na 3).

Mtunzi anakwenda moja kwa moja katika kueleza bintiye mawaidha yake bila kuzingatia utaratibu wa tenzi. Vilevile, utenzi wa *Howani Mwana Howani* una beti 398 tofauti na *Utenzi wa Mwana Kupona* ambao una beti 102.

Zaynab Himid Mohammed aliandika utenzi huu baada ya karne nzima tangu Mwana Kupona atunge utenzi wake. Utenzi wa *Howani Mwana Howani* ulitungwa mwaka wa 1983 nao *Utenzi wa Mwana Kupona* ulitungwa mwaka wa 1858. Kiwakati tenzi hizi zinatofautiana. Aidha, mazingira yao ya kijamii na kielimu na kiuchumi yalikuwa tofauti. Mwana Kupona alikuwa mke wa Sultan kwa hivyo tabaka lake lilikuwa la juu, pia, wakati alipotunga *Utenzi wa Mwana Kupona*, elimu iliyokuwepo ilikuwa ya dini na unyago au tohara. Aidha, mazingira halisi ya *Utenzi wa Mwana Kupona* yalikuwa Kisiwani Lamu nao utenzi wa *Howani Mwana Howani* ulitungiwa kisiwani Zanzibar.

Utenzi wa *Howani Mwana Howani* una wahusika kadhaa; Mamake Sihadaike, Sihadaike mwenyewe ambaye alizaliwa kutokana na malezi tuliyoelezwa katika utenzi wenyewe, wazazi wa mamake Sihadaike ambao hawajatajwa kwa majina, mkunga ambaye ni bibi yake Sihadike, mwalimu wa madrasa na wanajamii kati ya wengine. Ingawa tenzi hizi zilibainisha muumano kutokana na sababu kuwa watunzi walikuwa wa jinsia moja na waliwausia binti zao, kama alivyosema Bakhtin (1981), nguvu za Kani Pewa za lugha huathiri matini kwa kuifanya kubadilikabadilika. Utenzi wa *Howani Mwana Howani* umedhihirisha mabadiliko hayo ambayo yanakuwa upya katika muktadha wa wahusika kwa kuwa, katika utenzi huu kuna wahusika anuwai wakilinganishwa na *Utenzi wa Mwana Kupona* ambao ijapokuwa kuna wahusika waliorejelewa kama watumwa, mvuli, marafiki, baba, wahusika wanaochukua nafasi kubwa katika kufanikisha utenzi huo ni Mwana Kupona na bintiye. Aidha, ijapokuwa Zaynab na Mwana Kupona walikuwa wanawake na waliwausia binti zao, upya unabainika katika nyakati za utunzi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2066

mbali na mazingira tofauti ya watunzi, utangulizi na idadi ya beti.

Sehemu hii ilichunguza upya wa utenzi wa *Howani Mwana Howani* Mohammed (1983) ukiwemo dhamira ya mtunzi, maudhui mapya katika utenzi huo kama vile malezi ya mimba na kujifungua, malezi ya mtoto mchanga, tiba za kienyeji, sherehe za Waswahili na vipengele vya muundo vikiwemo muundo mazingira na wahusika. Sehemu itakayofuata itachunguza upya katika utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona* El-Maawy (2011).

**Utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona.***

Sehemu hii itachunguza upya katika utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona* El- Maawy (2011) ukiwemo wasifu wa mtunzi, dhamira ya mtunzi, maudhui yanayoonyesha upya kama vile ukakamavu katika kuzungumza na mume, haki za wanawake, radhi ya mume, kuomba ruhusa na majukumu mapya ya mke na upya wa vipengele vya muundo vikiwemo mazingira na uhusika.

**Wasifu wa Ali Abdalla Ali El-Maawy**

Utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona* ulitungwa na mzee Ali Abdala Ali El-Maawy. El-Maawy aliyezaliwa kisiwani Lamu mwaka wa 1929. Alisoma katika shule ya msingi ya kibinafsi akapata cheti ambacho kilimwezesha kuendelea na masomo yake ya shule ya upili ambayo pia ilikuwa shule ya kibinafsi. Alipata cheti cha shule ya upili ambacho kilimwezesha kujiunga na chuo cha ualimu kule Zanzibar. Alipata cheti cha ualimu wa shule za msingi mwaka wa 1952. Baadaye alikwenda Uingereza katika Chuo Kikuu cha Leeds ambapo alipata cheti cha utawala katika elimu ya msingi mwaka wa 1964. Alipata fursa ya kuendeleza masomo yake katika chuo hicho na kupata stashahada ya utawala katika elimu mwaka wa 1973. El-Maawy alikuwa mwalimu kuanzia mwaka wa 1953 hadi mwaka wa 1955. Baadaye alikuwa mwalimu mkuu kuanzia mwaka wa 1955 hadi mwaka wa 1959. Alipata fursa ya kuwa Afisa Msaidizi wa elimu, Mkurugenzi wa Elimu ya Mkoa, Afisa Mwandamizi wa Elimu, Mkaguzi wa Shule kabla kustaafu mwaka 1987.

Katika Utangulizi wa utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona*, Mutembei anamtambulisha El-Maawy kama Kitukutuku cha Mwana Kupona. Haya yanabainishwa na mtunzi katika Dibaji ya kwanza: (1395 A. H; 1976 AD) na katika ubeti wa 7-12 (El-Maawy, 2011). Mtunzi anaeleza namna aliona awe binti wa kuujibu *Utenzi wa Mwana Kupona*. Kwa kufanya hivyo alijitia Kitukutuku cha Mwana Kupona kisha kujiweka katika nafasi ya binti ili aupokee wasia. Kisha alijifanya binti ili kujibu beti zake Mwana Kupona. Baada ya kuchukua nafasi ya binti, aliweza kujibu beti za Mwana Kupona moja baada ya nyingine'. Kwa hivyo, utenzi huu ulitungwa na mwanamume ambaye alijitambulisha kama Kitukutuku cha Mwana Kupona katika kufanya hivyo, alijiweka katika nafasi ya mwanamke ili aweze kuujibu *Utenzi wa Mwana Kupona*.

**Dhamira ya Mtunzi**

El-Maawy (2011) naye aliandika utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona* zaidi ya miaka mia moja baada ya *Utenzi wa Mwana Kupona* kutungwa. Msukumo wa El- Maawy ulitokana na sababu kuwa maisha yalikuwa na mwisho hivyo basi aliona haja ya kueleza manufaa ya utenzi huo katika jamii. Hili lingewezekana kwa kutenda kwa kuwa alifahamu fika kuwa, binadamu asiyetenda alikuwa ni mfu. Ilikuwa muhimu kwake kutoketi tu na kuangalia. Hivyo basi, aliona haja ya kutunga utenzi kwa lengo la kuirithisha jamii mawazo yake ambayo yangebaki hai katika jamii.

Mambo mengi ya kigeni yalikuwa yameingia katika jamii hata kufanya mambo ya kale kusahaulika na kutothaminiwa. El-Maawy, aliona haja ya kuujibu *Utenzi wa Mwana Kupona* ili kuendeleza mafunzo yale kwa kuhifadhi yaliyokuwa muhimu ya wakati wake Mwana Kupona pamoja na kuonyesha yaliyopitwa na wakati kutegemea maendeleo ya jamii katika mpito wa wakati. Akizungumzia suala la 'Uanawake' (Womanism) kama inavyofafanuliwa na Ogunyemu (1985) na Kolawale (1997). El-Maawy (2011) anaonekana kushughulikia wanawake wa Kiafrika katika suala la kuhifadhi mawazo ya Mwana Kupona. Hii

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2066

inadhihirisha namna nguvu za Kani Kitovu zinavyofanya kazi katika kuhifadhi na kupokeza utamaduni wa jamii kuhakikisha kuwa anahifadhi utamaduni wa Waswahili ambao unastahili kuhifadhiwa huku akizingatia namna ya kukabiliana na mabadiliko ya kijamii ambayo yametokea katika jamii kutokana na mambo kama ukoloni ambao ulionekana kuathiri maisha ya wanawake wa Kiafrika.

Aidha, utawala wa Mkoloni uliathiri maisha na kuyabadili kwa sababu, Mkoloni alitawala siyo nchi peke yake, bali aliyatawala maisha, nyoyo na fikra za wanajamii. Waswahili walikuwa miongoni mwa wale walioathirika katika ada na mila. Ingawa haikuwa vizuri kupinga mapya yaliyofika katika jamii, lakini ilikuwa ni wajibu wa watu kuyahifadhi na kuyadumisha mema yao. Moja muhimu katika mema ya watu ni maisha ya kinyumbani. *Utenzi wa Mwana Kupona* na utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona* zilikuwa vyombo mwafaka vya kuyazindua na kuyadumisha mema hayo.

Katika kujibu *Utenzi wa Mwana Kupona*, El-Maawy alikusudia kuurejesha ule utukufu wa kizamani na kuulinganisha na hali ya kisasa. Kulingana naye, alijaribu asiyafiche maana ya mambo aliyoyausia Mwana Kupona hata kwa kiasi ambacho waliosoma hawangeridhika. Kwa mfano, zile beti zihusuzo uhusiano wa chumbani wa mke na mume (Allen, 1971: ubeti, 31 na 34).

Lililompa kufanya hivyo ni kujua kuwa, mila na desturi ya huduma ya mke na mume zinapotea na kwamba kuzificha ni kuzidi kuyasahau. Hilo ndilo lilikuwa kusudi la mtunzi alipotunga utenzi wake. Kwa hivyo, mawazo ya El-Maawy (2011) kuhusu dhamira iliyomsukuma kutunga ijapokuwa ilikuwa tofauti na ya Mwana Kupona kutokana na mpito wa wakati, ililenga kurejesha na kuhifadhi mapokeo ya jamii hasa kuhusu masuala ya unyumba ya Waswahili kama toleo la nguvu za Kani Kitovu. Acholonu (1995) anatumia dhana ya Ukinamama (Motherism) (tafsiri yetu) kuupanua mtazamo wake kwa wanawake wa Kiafrika kwa kuwapa wanawake wa vijijini au mashambani jukumu la kuikimu jamii. Vivyo hivyo, El-Maawy (2011) aliona haja ya kuhifadhi masuala ya unyumba kwa lengo la kuhakikisha kuwa jamii ilikuwa na utangamano ijapokuwa kulikuwa na mabadiliko mengi ambayo yalikuwa yametokea katika jamii.

Sehemu ifuatayo itashughulikia ukakamavu katika kuzungumza na mume, haki za wanawake, radhi ya mume, kuomba ruhusa, majukumu mapya ya mke na upya wa vipengele vya muudo katika utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona.*

**Ukakamavu katika Kuzungumza na Mume**

Katika utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona*, El-Maaawy (2011) anamuusia bintiye kuwa na adabu na ulimi wa thawabu na awe mtu wa kupendeka kila mahali atakapoingia (Allen, 1971, ubeti, 13). El-Maaawy (2011) aliona na akaridhia sababu ya ulimi mwema kama alivyopendekeza Mwana Kupona. Ezeigbo (2012) akifafanua Ufeministi wa hisia ya konokono (snail sense feminism) anasema, hii ni mbinu ya kutumia mazungumzo ya mwendo wa polepole ili kujadiliana na mume kwa lengo la kutatua matatizo ya kinyumbani kwa kutumia ulimi mtamu, ili kukabiliana na changamoto za nyumbani hata ziwe ni za kiwango kipi. Mwana Kupona anaokena kubobea katika kutumia ulimi wa thawabu. Vivyo hivyo, El-Maaawy (2011) anaunga mkono suala la kuwa na ulimi wa thawabu katika ndoa ili kuwa na uhusiano mwema kati ya mke na mke. Hata hivyo, El-Maaawy (2011) alikumbuka hali za kisasa za kuhitaji kuwa mkakamavu katika usemi na majibu katika hali ambazo kunyamaza kunampa nafasi dhalimu ya kuonewa (El- Maawy, 2011, ubeti, 54 na 55).

El-Maawy (2011) anasema ana wajibu kuwa mtu wa kupendeka na kutoyajibu maneno ila kwa yenye kusingiziwa. Kulingana naye, wanadamu wa siku hizi ukitaka kujitenga nao watakusingizia na ukiwa mwema, hukufanya dhaifu, muoga na mwenye hofu kiasi cha kukufanya kutoweza kujitetea. Mabinti wa sasa wanaweza kukusingizia kwa hivyo inahitaji ukakamavu wa kusema mhusika anapohisi kuwa amesingiziwa. Haya ndiyo baadhi ya mabadiliko ambayo yametokea katika jamii zaidi ya karne moja baada ya kutungwa kwa *Utenzi wa Mwana Kupona*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2066

kama toleo la nguvu za Kani Pewa. Mawazo haya yanaashiria mawazo tofauti na ya Mwana Kupona amabaye alitaka bintiye kunyamaza. Mabinti wa wakati huu hawatanyamaza kwa kusingiziwa. Watajitetea kwa kujibu mahali wanapohisi kuwa wamedhalilishwa.

**Haki za Wanawake**

Mwana Kupona alimuusia bintiye anyenyekee mbele za maqabaili na awaonapo mahali aharakishe kuwainukia (Allen, 1971, ubeti, 15). Kufuatia fikra hiyo, El-Maawy (2011) alikubaliana na Mwana Kupona aliposema akitaka ajifanye mnyenyekevu, mpole au mtulivu ni vyema. Yeye yuko radhi kuheshimu kila mmoja na wala hatastahimili kiburi. El-Maawy (2011) anaendeleza suala la heshima anaposema hatofanya ujeuri, atakuwa na hiari kuwaheshimu watu mwanzo na kiburi hatohimili. Atakuwa mtu wa maadili ambayo atayaweka kila mahali ili heshima idumu. Kulingana naye, atawaheshimu kila mmoja waungwana wa Swahili na kabila zote pia, wa karibu na wa mbali wenye wema wa vitendo. Hii inaonyesha nguvu za Kani Kitovu hasa ikizingatiwa kuwa heshima hii ameiweka kila mahali katika jamii.

Baadaye, El-Maawy (2011) anajibu vinginevyo tena kwa kusema, wanawake wa siku hizi waitaka haki kila mahali na kushika madaraka. Hata wanapokumbushwa kuwa haki za wanawake hazitimu peke yake ila washike wajibu katika kutimiza majukumu. Ndipo haki hizi zipatikane, hata wanaume wanastahili kufanya wajibu wao. El-Maawy (2011) anaendelea kushikilia kuwa, hilo litawezekana iwapo wanawake na wanaume watatimiza wajibu wao ili haki ipatikane. Iwapo wataheshimiana na kutendeana mazuri watajua kuwa wao wote ni sawa na hivyo kila mmoja kupata haki. Ongudipe (1994) anaona haya kama mabadiliko ya kijamii yanayowahusisha wanawake wa Kiafrika yaliyotokana na neno la Kiingereza STWA (Social Transformation Including Women in Africa). Katika muktadha wa utenzi huu, wanawake wanadai haki yao tofauti na nyakati za Mwana Kupona. Wao pia wanadai heshima kutoka kwa wanaume iwapo wanaume watataka kuishi kwa amani. Wanawake wanaonyesha mwamko wa kiharakati zaidi tofauti na ule wa Mwana Kupona kama toleo la nguvu za Kani Pewa.

Akishadidia haya, Stoeltje (2015) anasema, mabadiliko haya katika jamii ya karne ya 19 na 20 yameletwa na nguvu kutoka nje. Nguvu hizi ni kama ukoloni, Dini, mchakato wa usasa, kuondoka kwa wakoloni na mataifa ya Kiafrika kupata uhuru. Maingiliano haya yaliathiri wanawake kwa njia mseto: hasi na chanya. Katika jamii za Kiafrika wanawake wasomi wanaweza kuwa na mamlaka katika uongozi. Akiangazia suala hili, El- Maawy (2011) anasema wanaume wangali na nafasi kubwa katika masuala ya ndoa kwa kuwa mamlaka haya yanatokana na utamaduni wa Mwafrika. Mwanamke wa kisasa aitetea haki, usawa na kuwa huru, kwa viwango vya uzunguni ambavyo havikuwepo mpaka karne ya kumi na nane, na kutiliwa nguvu na umoja wa madola katika karne ya ishirini

**Radhi ya Mume**

Mwana Kupona alimuusia bintiye kuhusu kuwa mke mwema. Alianza kwa kumwambia kuwa asikilize maneno kwa kuwa kiumbe ni radhi tano ndipo apate amani ya akhera na dunia. Alikariri radhi hizi kwa kubainisha waliotoa radhi. Radhi ya kwanza ni ya Mungu na Mtumewe. Kisha baba na mama na ya tano ni ya mumewe ambayo imekaririwa mno (Allen, 1971, ubeti, 22 na 23).

El- Maawy (2011) anaunga mkono maneno ya Mwana Kupona kuhusu radhi za Mungu, Mtume wake, baba na mama kama toleo la nguvu za Kani Kitovu kwa kuwa kulingana naye, hawa wanaostahili kutoa radhi wamerasimishwa na kwa hivyo mafunzo haya yanafuatwa kama mwongozo kwa kuwa yanatolewa katika Kurani. Pia, jambo hili linathibitisha jinsi dini inavyochukuliwa katika jamii hii kwa uzito. Hata hivyo, upya unabainika pale anapopinga ile radhi ya mumewe kwa kusema kuwa, hii ya tano ambayo ni ya mumewe ni kwa wote mke na mume wala si baadhi. Anauliza ni vipi mume gharadhi anaweza kutoa radhi akimletea mazito. Kulingana naye, mume kama huyu hastahili kupewa wajibu wa kutoa radhi (El- Maawy, 2011, ubeti, 104).

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2066

Akishadidia mawazo haya, Nana (2010) anasema, kama mkakati wa kushughulikia maudhui ya kifeministi katika maudhui mapana ya kisiasa na ukombozi wa mataifa ulivyokuwa mkakati wa kiitikadi katika riwaya za Kiafrika katika miaka ya 1960 na 1970, wahakiki wengi wa wakati huo wakiwemo Frantz Fanon na Amilcar Cabral waliona kuwa, ni katika mageuzi ya kisiasa ndipo mahusiano mapya na urazini mpya unaibuliwa. Katika miktadha kama hiyo, Fanon anaelezea suala la mabadiliko ya utamaduni kwa kusema kuwa, utamaduni ni kitu kiyowevu na kinaingiliwa kati na nguvu za Kani Pewa. Mawazo haya yanashadidia yale ya El-Maawy (2011) anayepinga masuala ya utamaduni na kuhimiza haja ya kubadilika kama toleo la Kani Pewa. El-Maawy anasisitiza kuwa radhi haitatolewa na mume pekee hata mke ana wajibu wa kutoa radhi.

Mwana Kupona anamuusia bintiye awe radhi kwa mumeo siku zote wakaazo mpaka siku atakapochaguliwa awe amempa radhi (Allen, 1971:-ubeti, 24). El-Maawy (2011)

Akiitikia katika ushauru huu anauliza ni vipi mwanamume mgomvi asiyefanya mazuri aweze kumpa mke wake radhi. Anahoji kuwa, wakati wa Mwana Kupona waume walikuwa wema kwao na kwa hivyo, walihitaji kuwawekea utukufu wao. Kulingana na El-Maawy, leo ni mwenye bahati kupata mume wa dhati aliye na sifa za kutimia (El-Maawy, 2011:- ubeti, 108 na 109). Maoni ya El-maawy yanadhihirisha upya kutokana na maendeleo ya jamii. Ni vigumu kumpata mume aliye na sifa kama za wanaume wa wakati wa Mwana Kupona. Hii inaonyesha mabadiliko katika jamii hasa kuhusiana na malezi kama toleo la Kani Pewa.

Mwana Kupona anamuusia bintiye kuwa, iwapo ni mke atatangulia kufa, aitafute radhi ya mumewe aende kama ameibeba ndipo apate njia. Mumewe akipenda aende peponi atakwenda mara moja na akinena aende motoni hana budi atatiwa motoni (Allen, 1971, ubeti:- 26 na 27). El-Maawy (2011) anakubali kuwa mume ana nguvu mbele ya Mungu na kweli akipenda aende peponi ataenda. El-Maawy anasema kuwa, akipotoka au akifanya mambo mabaya kweli atakwenda motoni. Hata hivyo ana hofu kuwa, waume wote si sawa kwa kuwa kuna wengine wadhalimu ambao wanaweza kumtaka kwenda motoni. El-Maawy badala yake anaomba Mungu kumwepusha na watu wa wabaya. Hata hivyo, El-Maawy anasema wazi hata ingawa alimchagua mume atakaa naye kwa muda na akichoka na huyo mwanamume mdhalimu, atamshitakia kwa Mungu na kwa wazee; vilevile anaongezea kuwa, akichoka atakwenda kwa wazazi wake aende kuwashitaki bila kutangaza maneno yake kwa umma. Iwapo habadiliki na hataki kusikia nasaha ya wazee hana budi kushitakia mahakama ya sheria (El- Maawy, 2011, ubeti, 127 na 001).

Mawazo ya El-Maawy yanabainisha upya katika jamii. Kwanza kwa kupewa nafasi ya kumchagua mume, kuweza kumshtaki kwa Mungu, wazazi na sheria. Haya ni mawazo yanayoonyesha mabadiliko ya kijamii yanayowahusisha wanawake wa Kiafrika. Kama alivyoshikilia Ongudipe (1994), mabadiliko haya yanonyesha haja ya jamii kubadilika ili kuhusisha wanawake na keleta umoja kati ya wanaume na wanawake katika kafanikisha utangamano wa jamii katika karne ya ishirini na moja.

Katika *Utenzi wa Mwana Kupona* Allen (1971), Mwana Kupona anamwomba bintiye anene na mumewe bila kujibizana na ajitahidi kunyamaza. Anaongezea kuwa aende na mumewe kwa amani atakalo asimnyime wala wasishindane naye kwa kuwa mshindani huumia (Allen, 1971:- ubeti, 28 na 29). El-Maawy (2011) anaunga mkono maneno ya Mwana Kupona kama toleo la nguvu za Kani Kitovu ambazo zinafanana na Ufeministi wa hisia ya konokono (snail sense feminism) kama ilivyofafanuliwa na Ezeigbo (2012). Kulingana na Ezeigbo, ni kutumia mwendo wa polepole ili kujadiliana na mume kwa lengo la kutatua matatizo. El-Maawy (2011) anasema kuwa, hatokuwa na haja ya kumjibu mumewe na asemapo kwa ghadhabu, atatumia taratibu au atanyamaza ila wazungumzapo au wanapobarizi atakuwa mfunzi na mneni wa kuvutia ili aweze kumfanya kuelewa alichokuwa akitaka kwa kutumia ulimi mtamu, ili kukabiliana na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2066

changamoto za kinyumbani hata ziwe ni za kiwango kipi. El-Maawy na Mwana Kupona wanaelekea kukubaliana katika suala la kutumia lugha tamu katika kutatua matatizo ya nyumbani kati ya mke na mume (El- Maawy, 2011, ubeti:- 135). Kitukutuku anakubali kutoteta na mumewe kisha anaomba pia mume amwangalie vyema kwa kutimiza wajibu wake ili kufanya uhusiano huo ufaulu.

**Kuomba Ruhusa na Majukumu Mapya ya Mke**

Katika *Utenzi wa Mwana Kupona*, Mwana Kupona anamuusia bintiye kuishi kwa amani na mumewe. Binti anaambiwa, mume akitoka aagane naye na akiingia amkaribishe kisha amtengenezee mahali pa kupumzika. Mke anastahili kuwa nyumbani ili amuage mume pamoja na kumkaribisha. Akiendelea kueleza kuhusu jukumu hili, Mwana Kupona anamuusia bintiye asitoke bila ya kupata ruhusa ya mumewe na iwapo huku kutoka kutamuudhi mume wake asitoke (Allen, 1971:- ubeti 44).

Katika kujibu wasia wa Mwana Kupona, El-Maawy (2011) anapinga mawazo haya ya kusubiri kuomba ruhusa ili kutoka nyumbani. Kulingana naye, ruhusa ataomba anapotaka kutoka. Ila mumewe hana haja kuudhika kwa jambo lenye maana (El- Maawy, 2011:- ubeti wa 234). Suala linalomkabili mke wa kisasa ni kuwa ikiwa ni kwa haja ya dharura na mume yuko kazini, na harudi mpaka usiku na labda hakuna mawasiliano kwa sababu moja au nyingine, anaweza akatoka. Hivi ni kusema kwamba, mume hana haja kuudhika kwa jambo lenye maana. Yule mke ndiye hakimu bora zaidi wa hali yake. Ni kwa jambo lisilo sawa ndipo mume atakuwa na haki ya kuudhika. Hata hivyo, mawasiliano ya sasa ya simu za mikononi, mke anaweza kuwasiliana na mumewe popote alipo.

El-Maawy (2011) anasema kuwa katika nyakati za sasa mwanamke lazima atoke aende kazini. Anaongezea kuwa, huu ni wakati wa kuitaka senti na wanawake hufanya kazi ili kuwasaidia wanaume wao. Wao wanashikana kuwachumia wana wao na wanahitaji kufanya hivyo wakiwa vijana kabla uzee kuingia (El-Maawy, 2011, ubeti:- 235 na 236). Iwapo hili halitamfurahisha mume basi watakaa washauriane ili wajue ni lipi zuri. Hata hivyo, mume anastahili kujua kuwa siku hizi wanawake lazima watoke. Hii ni kwa kuwa wamesomea kazi mbalimbali za udereva wa kuendesha magari, baluni, wako shuleni kama walimu na ofisini wanafanya kazi. Huu sio wakati wa mke kukaa mekoni (El-Maawy, 2011:- ubeti wa 245). Wanawake wanataka wahesabike kwa mazuri na kujitosheleza. Mawazo haya yanaonyesha upya kama toleo la nguvu za Kani Pewa kwa kuwa nyakati zimebadilika tangu enzi ya Mwana Kupona. Wanawake wamekwenda shuleni na sasa wanataka kufanya yale yote wanayofanya wanaume.

Suala la kuchunga sheria, kuomba ruhusa, utangamno katika ndoa kati ya mengine ni maudhui mapya ya wakati wake El-Maawy yaliyotokana na nguvu za Kani Pewa za lugha zinazoonyesha tofauti na masuala aliyoshughulikia Mwana Kupona wakati wake.

**Upya wa Vipengele vya Muundo katika utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona.***

El-Maawy na Mwana Kupona ni watunzi kutoka Lamu, hata hivyo utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona* wa El-Maawy (2011) unabainisha upya kutokana na sababu kuwa El-Maawy alitoka katika mazingira tofauti kiwakati. Mwana Kupona alitunga *Utenzi wa Mwana Kupona* katika karne ya kumi na tisa (1858) naye El-Maawy alitunga utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona* katika karne ya ishirini (mwaka wa 1976). Kazi hii ilichapishwa mwaka wa 2011. El-Maawy anasema kuwa, uzuri wa utenzi huu ni kiungo kinachounganisha karne zilizopita na hizi za sasa. Katikati ya karne ya kumi na tisa fahari ya utamaduni wa Mswahili ulikuwa ungali, mwendo wa watu wa karne za nyuma ulikuwa bado unafuatwa, na mawazo ya Uswahili yalikuwa bado yana nguvu (El- Maawy, 2011, ubeti, 3 na 4).

Utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona* El-Maawy (2011) una muundo tofauti kwa kuwa umetungwa kwa namna ya kujibizana (ngonjera). Mtunzi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2066

anaujibu *Utenzi wa Mwana Kupona* ubeti baada ya ubeti. Mtindo huu ni ubunifu wa kipekee wa mtunzi katika mazingira ya wakati wake kama toleo la nguvu za Kani Pewa. Aidha, tofauti na *Utenzi wa Mwana Kupona*, utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona* una idadi ya beti 575 ukijumlishwa na *Utenzi wa Mwana Kupona*.

Wahusika katika utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona* (2011), ni mtunzi anayeitwa Ali Abdala Ali El-Maawy ambaye anajitambulisha kama Kitukutuku cha Mwana Kupona. Mtunzi ni mwanamume ambaye alitoka katika ukoo wa Mwana Kupona. El-Maawy (2011) ambaye alijitambulisha kama Kitukutuku cha Mwana Kupona, alijifanya kuwa kijana ili aujibu *Utenzi wa Mwana Kupona*. Anasema alifasiri mawazo ya wakati wake Mwana Kupona na kuweka ya jamii ya sasa ambayo ilikuwa ya wakati wake. Kulingana naye, wanajamii wa sasa wamezisahau mila kwa kushika mila mbalimbali ambazo zimewafanya kuwa na rangi mbili: Ulaya na Afrika. Mtunzi anaonyesha ubunifu wa kipekee katika kuchukua nafasi ya kike na kuujibu *Utenzi wa Mwana Kupona*. Kwa hivyo, upya katika utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona* unatokana na uhusika wa El-Maawy ambaye alikuwa mwanamume kama toleo la nguvu za Kani Pewa zinazoleta mabadiliko katika matini.

Sehemu hii ilichunguza upya katika utenzi wa *Jawabu la Mwana Kupona* (2011) ukiwemo wasifu wa mtunzi, dhamira ya mtunzi, maudhui yanayoonyesha upya kama vile ukakamavu katika kuzungumza na mume, haki za wanawake, mazungumzo kati ya mke na mume, kuomba ruhusa na majukumu mapya ya mke na upya wa vipengele vya fani vikiwemo mazingira, muundo na uhusika.

## HITIMISHO

Makala haya yalilenga kuchunguza upya wa Mwana Kupona katika utenzi wa *Howani Mwana Howani* na *Jawabu la Mwana Kupona*. Ilibainika kuwa upya ulijitokeza katika njia anuwai zikiwemo maudhui na muundo. Aidha, ilibainika kuwa, upya huo ijapokuwa uliwaathiri wanajamii husika, waliukubali katika muktadha wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa kuhakikisha kuwa upya uliokusudiwa ulilenga kumkomboa mwanamke katika mipaka ya kuhifadhi taasisi ya ndoa katika muktadha wa Kiafrika.

## MAREJELEO


Acholonu, C. O. (1995). *Motherism: The Afrocentric Alternative to Feminism.* Owerri: Afa Publications.

Allen, J. W. T. (1971). *Tendi*. Nairobi: Heinemann.

Bakhtin, M. (2001). *Discourse in the Novel. Modern Literary Theory*. 4th Edition. London: Routledge.

Bakhtin, M. M. (1981). *The Dialogic Imagination: Four Essays by M. M. Bakhtin* (Holquist, M. ed. Emerson, C. & Trans.).

Bayu, E. K. (2019). "A comparative analysis on the perspectives of African Feminism

Vs Western Feminism": philosophical debate with their criticism and its implication for women's rights in Ethiopia context. *International Journal of Sociology and Anthropology* Vol.11 (4), pp. 54-58, July-September 2019. http://www.academicjournals.org/IJSA

Beasley, C. (1999). *What is Feminism? An Introduction to Feminist Theory*. Available at: https://philpapers.org/rec/BEAWIF-2

Beja, S. K. & Mwinyifaki, A. (2013). 'Iktibasi' katika *Tenzi za Mwanakupona* na *Al-Inkishafi*. *Kioo cha Lugha*, *11*(1), 30-46. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Biersteker, A. (1991). "Language, Poetry and Power: A Reconstruction of 'Utendi wa Mwana Kupona.' In Harrow, K. W. (Ed.), '*Faces of Islam in African Literature'*. pp 37-58. London: James Currey.

Brandist, C. (2002). *The Bakhtin Circle: Philosophy, Culture and Politics*. London: Pluto Press.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2066

Chioma, F. S. (1981). T*he Black Woman Cross-Culturally*. Cambridge, Mass: Schenkman Publishers.

El-Maawy, A. A. A. (2011). *Jawabu la Mwana Kupona*. Dar es Saalam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Ezeigbo, A. (2012). *Snail-sense Feminism: Building on an Indigenous Model*. Lagos:

Gibbe, A. G. (1995). Inkishafi: Uhakiki wa Kidayakronia. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Moi. Eldoret. (Haijachapishwa).

Hirschkop, K. & Shepherd, D. (Eds.). (2001). *Bakhtin and cultural theory*. Oxford: Oxford University Press.

Holquist, M. (2002). *Dialogism: Bakhtin and His World*. London: Routledge.

https://btk.ppke.hu/uploads/articles/135505/file/introduction/satellite/literature_and_tradition.html retrieved on 27th March 2018. Islam International Publications.

Khatib, M. S. (1985). '*Utenzi wa Mwana Kupona*' katika *Mulika*. Na. 17: 46-52. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kolawole, M. M. (1997). *Womanism and African Consciousness*. Eritrea: Africa World Press.

Mbaabu, I. (1985). *Utamaduni wa Waswahili.* Nairobi: Kenya Publishing and Book Marketing Co. LTD.

Mbayi, L. A. (2009). Uhakiki wa Fani Katika Tenzi za *Howani Mwana Howani na Mwana Kukuwa* za Zaynab Himid Mohammed. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Nairobi. (*Haijachapishwa*).

Mdee, J. S., Njogu, K. & Shafi, A. (2011). *Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja*. Nairobi: Longhorn.

Mohamed, F. A. (2016). Kuchunguza Mila na Desturi za Mwanamke wa Visiwani Pamoja na Fani katika Tenzi za *Howani na Mwana Kukuwa*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (*Haijachapishwa*).

Mohammed, Z. H. (1983) 'Howani Mwana Howani-Kitunguu na Ubani' katika *Kiswahili* Vol 50/2. 70-91.

Momanyi, C. (2007). 'Patriachal Symbolic Order: The Syllables of Power as Accentuated in Waswahili Poetry.' In *The Journal of Pan African Studies*, Vol. 1, No. 8. Pg. 12-32. California: California Institute of Pan African Studies

Mulokozi, M. M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar-es-salaam: TUKI.

Munyole, S. D. (2017). Usomaji na Ufasiri Sasa wa *Utenzi wa Mwana Kupona*. Chuo kikuu cha Kenyatta. Tasnifu ya Uzamili (*Haijachapishwa*).

Njozi, H. M. (1990). *Utendi wa Mwana Kupona* and Reception Aesthetics. *Kiswahili,*

*57*, 55-67. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nana, W. (2010). "Feminism and Womanism". *A Concise Companion to Postcolonial Literature*. 120-140. Wiley Online Library.

Nnaemeka, O. (2004). Nego-feminism: Theorizing, practicing, and pruning Africa's way. *Signs: Journal of women in culture and society*, *29* (2), 357-385.

Nnaemeka, O. (2013). Foreword: Locating feminisms/feminists. *Feminist local and global theory perspectives reader. New York: Routledge*, 317-320.

Ogundipe, L. M. (1994). *Re-creating Ourselves: African Women & Critical Transformations.* Trenton, NJ: Africa World Press.

Ogunyemi, C. O. (1985). 'Womanism: The Dynamics of the Contemporary Black

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2066

Female Novel in English'. Signs: *Journal of Women in Culture and Society* 11(1): 63-80.

Opara, C. (2005). 'On the African Concept of Transcendence: Conflating Nature, Nurture and Creativity'. *International Journal of Philosophy and Religion.* 21(2): 189-200.

Stoeltje, B. (2015). *Women, Gender and the Study of Africa*. Oxford: New York.

Strobel, M. (1979). *Muslim Women in Mombasa. 1890-1975*. New Haven and London: Yale University Press.

Swaleh A. (1992). Maudhui Katika *Utenzi wa Mwana Kupona*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (*Haijachapishwa*).

Timammy, R. na Swaleh, A. (2013). 'A Thematic Analysis of Utendi wa Mwana Kupona: A Swahili Islamic Perspective' In *Journal of Education and Practice*. Vol. 4, No.28: 60-72.

Tong, R. (2009). *Feminist Thought: A More Comprehensive Introduction.* Colorado.

University of Lagos.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wandera, S. P. (1996). "Usawiri wa Mwana Kupona Katika Ushairi wa Kiswahili: 1800-1900; Uhalisi au Ugandamizwaji? Tasnifu ya M. A; Chuo Kikuu cha Egerton. (*Haijachapishwa*).

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.